# MUNGU rahisi ya wokovu ya

## Utangulizi

**Biblia imeelezea wazi wazi kwamba unaweza kujua kwa hakika baada ya kufa unaweza kwenda mbinguni. Swali ni Je? Wewe unaamini kile Mungu amesema kwa neno lake?**

1 Yohana 5:13 “Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele, ninyi mnaoliamini Jina la Mwana wa Mungu.”

## I Mimi Sisi sote ni wenye dhambi

**Si vigumu kwetu kukubali ya kwamba tumetenda mambo ambayo tunajua ni makosa, lakini hata hivyo, tunayatenda. Hiyo ndio inaitwa dhambi! Sisi tuna hatia kwa hiyo na tumekuwa tumekuwa tukitenda hivyo tangu kuzaliwa.**

Warumi 5:12 Kwa hiyo, kama kwa mtu mmoja dhambi iliingia ulimwenguni, na kwa dhambi hiyo mauti; na hivyo mauti ikawafikia watu wote kwa sababu wote wamefanya dhambi;

Warumi 14:12 "Basi ni hivyo, kila mtu miongoni mwetu atatoa habari zake mwenyewe mbele za Mungu.

Warumi 3:23 “kwa sababu wote wamefanya dhambi, na kupungukiwa na utukufu wa Mungu;

Warumi 3:10 kama ilivyoandikwa, ya kwamba, Hakuna mwenye haki hata mmoja.



**Mimi Sisi sote ni wenye dhambi**

## II Kuna bei kwa ajili ya dhambi.

Warumi 6:23 Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.

Ufunuo 21:8 "Bali waoga, na wasioamini, na wachukizao, na wauaji, na wazinzi, na wachawi, na hao waabuduo sanamu, na waongo wote, sehemu yao ni katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti. Hii ndiyo mauti ya pili."

Ufunuo 20:12 - 15
12 Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao.
13 Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na Mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake.
14 Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto.
15 Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.

# III Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu.

Warumi 5:6 Kwa maana hapo tulipokuwa hatuna nguvu, wakati ulipotimia, Kristo alikufa kwa ajili ya waovu.

Warumi 5:8 Bali Mungu aonyesha pendo lake yeye mwenyewe kwetu sisi, kwa kuwa Kristo alikufa kwa ajili yetu, tulipokuwa tungali wenye dhambi.

Warumi 14:9 Maana Kristo alikufa akawa hai tena kwa sababu hii, awamiliki waliokufa na walio hai pia.

Warumi 6:23 Kwa maana mshahara wa dhambi ni mauti; bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu.



**Kristo alikufa kwa ajili ya wenye dhambi!**

# IV Wokovu Ni Zawadi ya bure, SI Kwa matendo mema. Wewe lazima neno la Mungu Kwa ajili yake, NA Yesu Imani peke yake!

Wokovu ni kumwamini na kumpokea Yesu Kristo kama mwokozi wako. Ni kuamini ukweli ya kwambaYesu alikufa msalabani ili alipe deni la dhambi zako. Nikuelewa ya kwamba wewe mwenyewe hakuna jambo unaweza kufanya ujiokoe mwenyewe na hivyo kumwamini Yesu kristo kabisa akuokoe, si kanisa yeyote

yaweza kukuokoa. Si ubatizo wowote, si kwa kutenda matendo mema, si kuishi maisya mema, si-- **KWA KUTENDA JAMBO LOLOTE MENYEWE!!**

Waefeso 2:8-9 Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu.

Tito 3:5 si kwa sababu ya matendo ya haki tuliyoyatenda sisi; bali kwa rehema yake, kwa kuoshwa kwa kuzaliwa kwa pili na kufanywa upya na Roho Mtakatifu;

Vitendo 4:12 Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo.




# V lazima kuweka imani yetu na matumaini katika Kristo ili kuokolewa.

Warumi 4:24 bali na kwa ajili yetu sisi mtakaohesabiwa vivyo hivyo, sisi tunaomwamini yeye aliyemfufua Yesu Bwana wetu katika wafu;

Warumi 10:9,10,13 Kwa sababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu huamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. kwa kuwa, Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.

*Ndio, ni rahisi! Huwezi kupata msamaha toka kwa Mungu. Huwezi kulipia msamaha wako toka kwa Mungu. Unaweza ku upokea tu, kwa imani, kupitia neema na huruma za Mungu. Kama unataka kumkubali Yesu Kristo kama mwokozi wako na kupokea msamaha toka kwa Mungu, hapa kuna ombi unalo weza kuomba.*

*Kwa kusema ombi hili au ombi lengine lolote lile haiwezi kukuokoa. Ni kwa kumwamini Yesu Kristo pekee ndiko kutaleta msamaha wa dhambi. Ombi hili ni njia ya kumwelezea Mungu imani yako kwake na kwa kumshukuru kwa kukupea msamaha.*

**“Mungu,**

**najua ya kwamba nimefanya dhambi kinyume chako na ninastahili adhabu. Lakini Yesu Kristo akaichukua adhabu niliyo stahili ili kwa kumwamini yeye nipate kusamehewa. Ninaziacha dhambi zangu na nina weak imani yangu kwako ili niokolewe. Ahsante kwa neema yako kuu/ya ajabu na kwa msamaha! Amina.”**

**Kama umeomba maombi hayo – kulingana na neon la Mungu – UMEOKOKA! HALELUYA**

Unaweza sema, hauhisi tofauti. Unathania nini? Wokovu wako hautengemei vile inavyohisi. **YOTE** yatengemea vile Mungu **ALISEMA.**
Mungu alisema kama utampokea na kumwamini Yesu Kristo utaokoka. Elewa hapa HAISEMI “uenda” ama “uenda ikawa” umeokoka – lakini yasema “utaokoka” **UEMOKOKA**!!
Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka. Warumi 10:13

Wewe umemwamini Bwana Yesu Kristo? Angalia vile Yohana 3:36 inasema, una MAISHA YA MILELE! Sio “inawezekana” ama “natumaini hivyo” – LAKINI UNAO WOKOVU – UMEOKOKA!
Anayemwamini Mwana anao uzima wa milele; asiyemtii Mwana hatakuwa na uzima wa milele, bali ghadhabu ya Mungu hubaki juu yake." Yohana 3:36

Rafiki, kama umeomba maombi haya na umempokea Yesu Kristo – UMEOKOKA! **Umefanya yale Mungu anasema ufanye – NA MUNGU HAWEZI KUSEMA UONGO!** Katika tumaini la uzima wa milele, ambao Mungu, ASIYEWEZA KUSEMA UONGO aliuahidi tangu milele. Tito 1:2